Machi 19, 2020

Wapendwa Familia za JCPS,

Tuanjua zimekuwa ni wiki za kushangaza na zisizotarajiwa kwako, watoto wako na familia nyngine ya JCPS. Tuliahidi kwamba tutakujuza kuhusu kinachoendelea wakati shule za JCPS zimefungwa na tunapambana na janga la COVID-19. Haya ndio mapya:

- Bodi ya Elimu ya Kaunti ya Jefferson ilifanya mkutano maalum Alhamisi usiku. Unaweza kutazama marudio ya mkutano huo hapa. Jambo kuu katika ajenda ni idihini ya mpango wa wilaya wa Agizo Isiyo na Asili (NTI). **Ikiwa** JCPS itakubali na kuamua mpang wake wa NTI, mtoto wako atakuwa akishiriki katika kujifunza kwa umbali kupitia mtandao. Utakuwa ukipokea baadhi ya mawasiliano katika wiki mbili zijazo yakieleza jinsi hilo kitatendeka.
- Wengi wenu wameomba usaidizi kufikia. Mkoba Jiditali wa mtoto wako kutoka kwa kompyuta zenu za nyumbani au simu za rununu. Hapa kuna video ambayo inakuonyesha jinsi. Utahitaji kutumia Google Chrome kama kivinjari. Ikiwa ungali una tatizo kujiunga, unaweza wasiliana na mtaalam wa JCPS wa TEKNOLOGIA kwa usaidizi.
- Bodi za JCPS za Uchaguzi ambazo zina shughuli za ziada za kusoma na mazoezi ya kila kiwango cha daraja yaweza kupatikana hapa. Tunaona na kusikia hadithi nyingi jinsi nyinyi na watoto wenu mnazitumia kusoma kila siku.
- Viwanda vyetu vya Kusambaza Chakula cha Dharura vina mafanikio makubwa. Tunasambaza zaidi ya 12,000 viamsha vinywa na vyakula vya mchana vya bure kwa watoto wa miaka 18 na chini, bila kuuliza maswali, kila siku ya wiki kutoka 10 asubuhi – 1 mchana. Hii ndio orodha ya vile viwanda 58 vya usambazaji na ramani ya viwanda katika Kaunti ya Jefferson.
- Washauri wa JCPS wameunda vidokezo kadhaa kusaidia familia kukabiliana na dhiki ya kukaa nyumbani kila siku.
- Majengo yote ya JCPS ikiwa ni pamaoja na Jengo la Elimu la VanHoose na Jengo la Lam zimefungwa kwa uma. Hii itaadhiri wazazi na walezi ambao wanajaribu kusajili watoto wao kibinafsi. Unaweza jisajili mtandaoni hapa. Maswali? Pigia 313-HELP kutoka 7:30 asubuhi hadi 5:00 jioni Jumatayu-Ijumaa.

Tutakujuza moja kwa moja kwa maendeleo yoyote yajayo vile yatakavyotendeka wakati huu usio wa kawaida. Asante kwa kumkabidhi mtoto wako kwa walimu wanaofanya kazi kwa bidii, wasimamizi na wafanyakazi katika JCPS.